Toleo Maalum

# jarida la WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Jarida la Mtandaoni | www.michezo.go.tz | Septemba 06, 2022



# Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo



# Watanzania Wamehamasika Kushiriki Tamasha la JAMAFEST

Na Eleuteri Mangi - WUSM

Balozi wa Tanzania nchini Burundi Mhe. Dkt. Jilly Elibariki Maleko amesema Watanzania wamehamasika na wamekuja kwa wingi katika Tamasha la Tano la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) linalofanyika kuanzia Septemba 4-12, 2022 nchini Burundi.

Mhe. Balozi Dkt. Jilly amesema hayo Septemba 06, 2022 mara baada ya kutembelea mabanda ya wajasiriamali kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki walioleta bidha zao kwenye hilo.

Nimemaliza kutembelea mabanda ya Tanzania na nchi nyingine, nimeona hamasha kubwa sana Watanzania waekuja kwa wingi, watu mbalimbali wameleta bidhaa za Sanaa, chakula na kwa sababu Burundi wanapenda sana bidhaa za chakula kutoka Tanzania. Nimeona jinsi wanavyochangamkia mchele, dagaa, viungo vya chakula, mafuta, nguo batiki, mapambo ya mwili na picha za Tingatinga, kwa kweli maonesho yamefana" amesema Mhe. Balozi Dkt. Jilly.

Mhe. Balozi Dkt. Jilly ameongeza kuwa ofisi yake inashirikiana pamoja na watanzania ambao wamekuja kweny tamasha hilo kwa kuwahamasisha watu mbalimbali wakiwemo Wtanzania waishio nchini Burundi, jamii ya kimataifa wakiwemo Mabalozi wanaoziwakilisha nchi zao, wafanyakazi wa mashirika pamoja na kikanda na kuwahimiza kutembelea mabanda yote ya nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Pamoja na maonesho hayo ya Sanaa na Utamaduni, mada mbalimbali ziliwasilishwa tamasha hilo kiwemo jukumu la teknolojia ya kisasa kwa kutumia utamaduni, tasnia ya sanaa na utalii, ushiriki wa vijana katika shughuli za sanaa katika jumuiya ya EAC pamoja na matokeo ya uvumbuzi katika sanaa na utamaduni.







# Kiswahili Kinakuza Diplomasia ya Uchumi Jumuiya ya Afrika Mashariki

Na Eleuteri Mangi - WUSM

Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) pamoja na Chuo Kikuu Huria cha Tanzania (OUT) kupita tawi lake la mkoa wa Kigoma kutumia fursa ya kufundisha Kiswahili nchini Burundi kwa kuanzisha programu fupi fupi za kufundisha lugha hiyo ili kukuza diplomasia ya uchumi miongoni mwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC).

Akichangia mada wakati wa wasilisho la mada ya "Lugha Ya Kiswahili Inamchango Mkubwa katika Kukuza Diplomasia ya Uchumi" Septemba 07, 2022 Bujumbura nchini Burundi, Balozi wa Tanzania nchini humo Mhe. Dkt. Jilly Elibariki Maleko amesema huu ni muda mwafaka kwa taasisi zinazofundisha Kiswahili kuongeza kasi ya kukuza na kueneza lugha hiyo miongoni mwa nchi za jumuiya hiyo.

Ili kukabiliana na hali hiyo, Mhe. Balozi Dkt. Jilly amesema ni muhimu kuwa na programu ya kufundisha walimu nchini Burundi ili waweze wao wenyewe kujitegemea katika kufundisha Kiswahili katika maeneo yao kuanzia ngazi ya shule za msingi, sekondari hadi Chuo Kikuu.

Aidha, Balozi Mhe. Dkt. Jilly amelitaka Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) ambalo ni taasisi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo pamoja na taasisi zinazojushughulisha maendeleo ya Kiswahili zisaidie katika kukuza na kueneza lugha hiyo miongoni mwa nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

"BAKITA na taasisi zingine zitusaidie sasa katika utekelezaji wa hati ya makubaliano ili tuweze kuwasaidia wenzetu wanahitaji walimu, tunasaidiana vizuri sana katika kuhamasisha matumizi ya Kiswahili hapa Burundi, tunashirikiana kwa karibu na Chuo Kikuu cha Burundi, wanahitaji sana walimu katika shule za msingi na sekondari ambapo hawana walimu wa Kiswahili kabisa" Mhe. Balozi Dkt. Jilly.

Akiwasilisha mada kuhusu lugha ya Kiswahili inavyoweza kukuza Diplomasia ya Uchumi kwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki wakati wa Tamasha la Tano la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) linalofanyika kuanzia Septemba 4-12, 2022 nchini Burundi, Dkt. Rizati Hassani Mmary kutoka Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) amesema Kiswahili kinakua kwa kasi katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kupitia miradi inayotekelezwa ikiwemo kufundisha Kiswahili kwa wageni, Muziki na filamu, biashara, utalii na hivyo kuwa na mchango mkubwa katika kukuza diplomasia ya uchumi miongoni mwa nchi wanachama wa jumuiya hiyo.

**Matukio mbalimbali ya Watanzania wakitoa burudani wakati wa Maadhimisho ya Tamasha la Tano la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) linalofanyika nchini Burundi kuanzia Septemba 4-12, 2022.**






BURUNDI









# Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo Yatekeleza Ahadi Waliyoitoa UMITASHUMTA

Na Eleuteri Mangi - WUSM

Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo imetekeleza ahadi waliyoitoa wakati wa Mashindano ya kitaifa ya Umoja wa Michezo na Taaluma Shule za Msingi Tanzania (UMITASHUMTA) mkoani Tabora kuwa mkoa utakaoshika nafasi ya kwanza Kitaifa katika fani ya ngoma watapewa fursa ya watashiriki Tamasha la Tano la Sanaa na Utamaduni la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) 2022.

Wanafunzi hao ambao ni washindi wa kwanza wa mashindano ya UMITASHUMTA katika fani ya ngoma wanatoka shule ya msingi Mwanyahina kutoka wilaya ya Meatu mkoani Simiyu Septemba 8, 2022 wametumbuiza kwenye Tamasha la JAMAFEST nchini Burundi.

Akizungumzia ushiriki wa wanafunzi hao, Mratibu wa Tamasha la JAMAFEST ambaye pia Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Sanaa nchini Bi Leah Kihimbi amesema wanafunzi hao ni miongoni mwa wanafunzi walioshiriki UMITASHUMTA 2022 na kuibuka kidedea katika fani ya ngoma.

"Hii ndiyo njia njema ya kuwafundisha watoto wetu hasa wanafunzi kupitia Sanaa ya ngoma za asili, wanafunzi hujifunza kujiamini, kukuza tabia njema ya kuishi na kuwa na maadili mema pamoja na kuimarisha na ushirikiano miongoni mwa wanafunzi wenzao na hatimaye taifa zima" amesema Mratibu huyo.

Akizungumzia mwaliko huo waliopewa na Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mwalimu Suzan Julius ambaye ameambatana na wanafunzi hao amesema kwao ni fursa nzuri ya kujifunza maana ni mazingira mapya na wanakutana na watu wengi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki ambao wamekusanyika nchini Burundi.

Kwa upande wake Manju wa ngoma hiyo ambaye pia ni mwanafunzi wa darasa la sita kutoka shule ya msingi Mwanyahina Musa Sita amesema ushindi wao katika mashindano ya UMITASHUMTA ndiyo umewapa tiketi ya kutumbuiza kwenye JAMAFEST nchini Burundi.

"Sina mengi ya kusema, ninafuraha sana. Nawashauri wanafunzi wenzangu kote nchini wafanye mazoezi na kushiriki kwenye Sanaa ili baadaye wawe wasanii wakubwa" amesema Sita.




# Balozi Mhe. Dkt. Jilly: Tunafursa ya kuitangaza lugha ya Kiswahili Kupitia Matamasha

Na Eleuteri Mangi - WUSM

Balozi wa Tanzania nchini Burundi Mhe. Dkt. Jilly Elibariki Maleko amesema Watanzania tunafursa ya kuitangaza lugha yetu ya Kiswahili katika matamasha mbalimbali duniani ili kukieneza kwa mataifa mengine.

Balozi Mhe. Dkt. Jilly amesema hayo Septemba 8, 2022 wakati akiongea na timu ya wawakilishi kutoka Tanzania Ofisini kwake Mtaa wa Kinindo Bujumbura nchini Burundi wakati wakiwa nchini humo kwenye Tamasha la Jumuiya ya Afrika Mashariki (JAMAFEST) ambalo linafanyika kuanzia Septemba 4-12 Bujumbura nchini Burundi.

"Kiswahili ni Bidhaa, tukitangaze kwa nguvu katika maonesho na matamasha yote kwa kukitengenezea mpango wa kukiuza kwa kuuza vitabu na bidha nyingine za Kiswahili. Kwa mfano hapa Burundi tuna Hati ya Makubaliano ya kufundisha Kiswahili na Burundi kufundisha Kifaransa nchini Tanzania" amesema" Balozi Mhe. Dkt. Jilly.

Kwa upande wao Viongozi kutoka Tanzania Dkt. Emmanuel Ishengoma Mkurugenzi Idara ya Maendeleo ya Sanaa, Dkt. Emmanuel Temu pamoja na Mratibu wa Tamasha la JAMAFEST ambaye pia ni Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Sanaa Bi Leah Kihimbi wamesema Tanzania inauwakilishi mzuri kwenye Tamasha hilo ambapo takriban washiriki takriban 200.

Hati ya makubaliano ya kufundisha Kiswahili nchini Burundi na Kifaransa nchini Tanzania ilisainiwa baina ya Serikali za nchi hizi mbili mwezi Julai 2021 wakati wa ziara rasmi ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliyoifanya katika Jamhuri ya Burundi wakati huo.

Tanzania imewakilishwa kwenye Tamasha la JAMAFEST na washiriki kutoka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, taasisi zilizochini ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, kikundi cha ngoma cha wanafunzi kutoka shule ya msingi Mwanyahina kutoka wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, wasanii pamoja na wajasiriamali.



# Tanzania Yang'ara JAMAFEST Nchini Burundi Kwenye Sanaa za Jukwaani

Na Mwandishi Maalum

Tamasha la Tano la Jumuiya ya Afrika Mashariki la Sanaa na Utamaduni (JAMAFEST) limefungwa rasmi Bujumbura nchini Burundi kwa Burundi kukabidhi Bendera ya Jumuiya hiyo kwa Sekretarieti hadi itakapotangazwa nchi ambayo itakuwa mwenyeji wa tamasha la sita.

Katika Tamasha hilo, Tanzania imeendelea kufanya vizuri katika Sanaa za Jukwaani ambapo Septemba 9, 2022 Muziki wa taarabu umepeperusha vyema bendera ya Taifa kupitia kikundi cha Taifa cha Taarabu Asilia kutoka Zanzibar huku wasanii nguli wa muziki huo Abdul Misambano na Mzee Yusufu wakiibua shangwe na nderemo kutoka kwa washiriki wa tamasha hilo pamoja na wananchi wa Burundi waliofurika katika viwanja vya Intwari jijini Bujumbura.

Akizungumzia ushiriki katika Tamasha hilo, Mratibu wa JAMAFEST Tanzania ambaye pia ni Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Maendeleo ya Sanaa Bi Leah Kihimbi amesema Tanzania imefanya vizuri kwa kuwaleta wasanii wengi kwa fani mbalimbali ikiwemo taarabu, muziki wa Singeli, ngoma za asili ikiwemo wanafunzi wa shule ya msingi Mwanyahina kutoka wilaya ya Meatu mkoani Simiyu, Sanaa za Ufundi za uchongaji, uchoraji, wasusi, wajasiriamali pamoja na watumishi wa Umma.

Akifunga tamasha hilo Mgeni Rasmi ambaye pia ni Katibu Mkuu Wizara ya Masuala ya Afrika Mashariki, Vijana, Michezo na Utamaduni Burundi Bw. Severin Mbarubukeye amesema kuwa amefurahishwa kwa ushiriki wa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kwenye Tamasha la Tano JAMAFEST nchini humo.

Aidha, ameongeza kuwa linasaidia kuimarika umoja na mshikamano katika nchi wanachama kuwa sehemu moja kwa wakati mmoja kubadilishana na kujifunza uzoefu wa nchi wanachama kwenye masuala ya Utamaduni.

Tanzania katika tamasha la JAMAEFEST 2022 imewakilishwa na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Utamaduni Dkt. Emmanuel Temu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Sanaa Dkt. Emmanuel Ishengoma, Mtatibu wa Programu ya Ukombozi wa Bara la Afrika Bw. Bonifance Kadili, Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania Dkt. Kilonzo Kiagho pamoja na watumishi kutoka Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mkurugenzi wa Miundombinu ya Kiuchumi na Huduma za Usaidizi wa Kijamii Eliabi Khalid Chodota kutoka Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, watumishi kutoka Wizara ya Elimu, Sayansi na Tekniolojia, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Wizara ya Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, wajasiriamali pamoja na wasanii wa muziki, ngoma za asili, wachoraji na wachongaji.

Toleo
Maalum

# WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

## Limeandaliwa na Kitengo cha Mawasiliano Serikalini - GCU




## Mawasiliano

P.O. Box 25, Dodoma,Tanzania
Mji wa Serikali Mtumba
Telephone: +255 26 2322 129
Nukushi: +255 26 2322 128
Barua pepe: km@michezo.go.tz